**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/3 - FASIHI**

**KIDATO CHA TATU MUHULA WA TATU 2025**

**SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI**

**1. Lazima**

a i) Sifo/majigambo/vifugo. (alama 2x1=2)

b) i) Hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe.

ii) Hutungwa kwa usanii mkubwa.

iii) Anayejigamba hujitungia kivugo kufuatia tukio mahususi katika maisha yake.

iv) Kwa kawaida majigambo au vivugo hutungwa na kughanwa na wanaume.

v)Huwa na matumizi ya chuku.

vi) Majigambo hutolewa kwa nafsi ya kwanza kwa sababu anayejigamba huwa ni mshairi mwenyewe.

vii) Anayejigamba huwa kabeba baadhi ya vifaa vyake vya kazi au vinavyoonyesha Jambo analojisifia.

viii) Maudhui makuu katika majigambo huwa ni ushujaa.

ix) Wanaojigamba mara nyingi huwa walumbi au washairi wanaoelewa kwa kina wanalolitongoa.
(alama 6x1=6)

b i)Kuonyesha hisia usoni.

ii) Kuuliza na kujibu maswali.

iii)Kuimba nyimbo.

iv) Kupiga makofi.

v) kutoa majibu ya methali iwapo itadokezwa na mtambaji.

vi) Kuigiza baadhi ya vitendo katika masimulizi.

vii) Kuitamba upya ngano hiyo.

viii) Kuitikia Kwa kichwa.

ix) Kunakili hoja muhimu (alama 6x1=6)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

c) Changamoto

(i) Tatizo la kimawasiliano huenda likaathiri utoaji wa habari.

(ii)Huenda mhoji/mhojiwa asiwe na muda wa kutosha wa mahojiano.

(iii)Mhojiwa kumshuku mhoji,hivyo kutotoa habari za kutegemewa.

(iv)Mhoji kuwajaza wahojiwa hofu kutokana pengine na kiwango chake cha elimu.

(v)Kwa vile wahojiwa wanakabiliana na mhoji moja kwa moja,huenda wakampa habari za uongo ili kumfurahisha.

(vi)Ikiwa matini ya mahojiano imeandikwa kwa lugha tofauti na ajuayo mhoji, huenda pakawa na tatizo la kutafsiri.

(vii)Ni njia ghali kwani kwa kawaida mtafiti sharti asafiri kukutana na mhojiwa.

(viii)Anayehoji akishindwa kuibua maelewano baina yake na mhojiwa mwanzoni, huenda mawasiliano yakatizwe,hivyo kuathiri vibaya utoaji wa habari.

*(alama 6x1=6)*

**SEHEMU B: TAMTHLIA**

**Bembea ya Maisha**

2 a) Mawazo/ uuzungumzaji nafsi wa Neema(i),akimwazia mamake mzazi Sara(ii)

Yuko sebuleni/ nyumbani kwake(iii).

Baada ya Neema na Bunju kuwa na majibizano kuhusu mila na tamaduni na jinsi haikukubali mama au baba mkwe kulala kwa wanawe.(iv) (alama 4x1=4)

**b) Mbinu za lugha**.

i) Sitiari-mboni ya jicho-mwangalizi wao

ii) Msemo/nahau-lala salama

iii) Usiahi/nidaa-mama!

iv) Taswira oni-mboni ya jicho *za kwanza tatu (3x1=3)*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

c) *Sifa za Sara (Mamangu mzazi)*

1. Mvumilivu: Sara alivumilia mateso ya mume wake ambaye alimlaumu kwa kutopata mtoto wa kiume.

2. Mpatanishi: Sara ni mpatanishi kwa kuwa alimshauri bintiye amwelewe mume wake ambaye alitii.

3. Mwenye utu: Sara aliijali ndoa yake na kumpenda mumewe licha ya fujo zake. Alikataa kukaa mjini.

4. Mwenye hekima: Maneno anayozungumza yana wingi wa hekima na busara. Anamweleza Asna asicheze na akili zake ijapokuwa hakupata elimu sawasawa.

5. Mlezi mwema: Anawalea wanawe kwa kuwapa mawaidha ya busara.

6. Mtamaduni: Neema anatilia maanani tamaduni za jamii yake. Kwanza tunamwona akisema kuwa fimbo hurithiwa na mtoto wa kiume.

7. Mwenye uhusiano mwema: Sara alikuwa na uhusiano mwema na Dina. Anapougua, Dina anakuja kumsaidia kwa kuwa walikuwa na uhusiano mwema.

8. Mwenye msimamo thabiti: Hata baada ya kusutwa na kukejeliwa na wanajamii hakuyumbishwa na maneno yao.

9. Mvumilivu.Sara anavumilia mateso ya kuchapwa na mumewe. (alama 6x1=6)

**d) Majukumu ya elimu katika jamii kwa mujibu wa Tamthilia ya Bembea ya Maisha.**

i) Elimu huzidua jamii kutofuata mila potovu-Neema msichana wa kike kuwa mwanga kijijini.

ii) Inasaidia kupata ajira-Yona aliajiriwa kuwa mwalimu kutokana na kisomo chake.

iii) Chombo cha maendeleo na ufanisi-Neema anaendesha gari,anajengea wazazi wake nyumba kupitia Bunju.

iv) Elimu hufinyanga maadili-Elimu ya dini ilimfanya Yona kuwa mwaadilifu kabla ya kuingilia ulevi.

v) Hupalilia vipawa-Lemi walikuwa wanafanya mazoezi ya nyimbo kwa ajili ya siku ya wazazi shuleni,Lemi akitoka shuleni lazima amuonyeshe Bela miondoko na minenguo yote waliofanya pale shuleni.

vi) Elimu humsaidia binadamu kuishi na kutatua matatizo yake.Bunju anatatua matatizo ya familia ya Neema kwa ufadhili kutokana na mshahara wake na mikopo.

vii) Inasaidia mwanamke kuolewa

viii) Kurekebisha tabia. *(alama 7x1=7)*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

3 a) i) Nidaa-si neno mama!

ii) Tashbihi-mfano wa mbegu

iii) Istiari/jazada-mbegu

iv) Msemo-haina budi.

v) Uhuishi/tashhisi-mazuri hutoka mbali ***kutaja 1mfano 1 za kwanza nne*** **(alama 4x2=8)**

b) **Umuhimu wa Sara**

i) Ametumika kuonyesha wanawake wavumilivu/wastahimilivu.

ii) Ametumika kuonyesha mwanamke mwenye hekima anakabiliana na changamoto zote za maisha.

iii) Kuonyesha ulezi bora wa watoto.

iv) Kutumiwa kutuonyesha mtu ambaye ni mtetezi mzuri k.m. anamtetea mume wake kwa watoto wake.

v) Mpenda amani.

vi)Mwenye bidii ya kazi. Anamsaidia mume wakekusomesha watoto kwa kujishughulisha na uuzaji wa maziwa na mazao ya shambani.

vii) Mwanamke mwenye ujasiri. Hajuti uamuzi wake wa kuvumilia mateso na kupata ugonjwa wa moyo.

viii) Ametumiwa kama mwanamke msema ukweli. Anawaambia watoto wake kwamba familia yake haikuwa na mali. (alama 6x1=6)

c) **Mikakati ya kujikomboa kutoka utamaduni.**

i) Wanawake kupata elimu k.v. Neema na Asna.

ii) Wanawake kufanya kazi k.v. Neema

iii) Wanawake kuendesha magari k.v. Neema anaendesha gari mjini na pia anamwendea mamake kijijini kumpeleka hospitalini kwa gari.

iv) Yona anaacha kumpiga mkewe na kuahidi kuanza kumtunza.

v) Wazee wanaanza kushughulikia majukumu ya nyumbani.Yona anaanza kuingia jikoni kupika na kumsaidia Sara.

vi) Wanajamii wamebadili mila ya kuoa wake wengi ili wapate mrithi.Yona anakataa kuoa mke mwingine baada ya kukosa mtoto wa kiume kama mrithi. *za kwanza sita* (alama 6x1=6)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Riwaya.**

**Nguu za Jadi**.

4.a) Maneno ya mwandishi(i) akimrejelea Mangwasha alipokuwa akiota(ii) nyumbani kwake(iii).Mangwasha alikuwa amekataa mlungula wa Sagilu aliyekuwa amemtembelea kwake.Ndiposa alipolala akaota jinyama lililokuwa likitoa moto likimkimbiza.(iv)

*(alama 4x1=4)*

b) i) Swali balagha- Sasa afanye nini?

ii) Taswira- …Alilitupia lile jinyama lakini likahepa.

*(alama 2x2=4)*

b) i Kujenga ploti mfano, waketwa wanaporudi makwao.

ii) Kutambulisha wahusika mfano Sagura, Sauni, Mkuu wa polisi.

iii) Kujenga sifa za wahusika mfano Sauni - hasira, Lonare – busara

iv) Kujenga maudhui mbalimbali mfano; ukatili, utetezi wa haki.

v) Kubainisha mgogoro unashamiri kati ya makundi mawili hasimu (waketwa na serikali) (Sauni na mkuu wa polisi).

vi) Kuchimuza dhamira ya mwandishi kuwa wanajamii wana jukumu la kutetea haki zao dhidi ya viongozi dhalimu.

vii) Kufunza kuhusu mbinu chanya za kusuluhisha migogoro. Lonare anamhimiza Sauni aachane na wale polisi.

*hoja zozote sita ( alama 6x1=6)*

**Tanbihi**

*Mtahiniwa akikita hoja zake kwenye mandhari moja tuu kama vile ofisini mwa Chifu Mshabaha atuzwe mradi ametosheleza hoja.*

d i) Mwanamke anaonekana kama chombo tu cha kuchuuzwa na mwanamume. Baadhi ya Waketwa waliochomewa nyumba zao wanatoa hoja kuwa kuna wale waliowauza wake zao kwa wakuu ili wapate ajira.

ii) Wanawake hawana sauti mbele ya wanaume kama anavyowaza Mangwasha kuwa "...walipaswa kusikiliza na kutenda bali si kusikilizwa na kutenda." (uk. 11).

iii) Utamaduni unamfunza mke kujitegemea katika maisha bali si kumtegemea mume kujikimu katika maisha yake.Mbungulu anamshinikiza Mangwasha kujitahidi kukidhi mahitaji ya wanawe.

iv) Mrima anaamini kuwa mwanamke huwa na maneno mengi kama chiriku na kwamba mke hapaswi kumuuliza mumewe kule aendako au atokako.

v) Mrima anamwaambia Mangwasha kuwa ,yeye ni mwanamume na mke hangemzuia kuoa; kwamba angeweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

vi) Utamaduni asilia pia unamtaka mume aweze kuitunza jamaa yake pamoja na kuisimamia. Hii ndiyo maana Mrima anasisitiza kuwa mila haimruhusu kutunzwa na mkewe.

vii) Mila hairuhusu mwanamke kumfuata katika vyumba vya starehe.Mbungulu anamweleza Mangwasha kuwa hastahili kumfuata Mrima katika vyumba vya starehe. *hoja za kwanza sita sahihi.(alama 6x1=6)*

5**.a) Umuhimu wa Lonare**

i) Anawakilisha viongozi wanaozingatia demokrasia na haki za wananchi.

ii Kupitia kwake, wananchi wanakuwa na imani ya uongozi mzuri na matumaini katika maisha yao.

iii) Ni kielelezo cha watu wasiokata tamaa maishani.

iv) Ametumiwa kuonyesha jinsi ushirikiano miongoni mwa wananchi unavyoweza kubatilisha uongozi dhalimu.

v) Ametumiwa kama chombo cha kuleta mabadiliko katika utawala usioridhisha. Mtemi Lesulia.
*zozote nne (alama 4x1=4)*

b) i.Unyakuzi wa ardhi ya wanajamii. Sagilu anapanga kunyakua ardhi ya wanamatango.

ii.Kufutwa kazi kiholela. Mangwasha anapigwa kalamu katika ofisi ya chifu kwa kuunga mkono kampeni za Lonare.

iii.Mshahara mdogo kwa wafanyikazi. Mshahara anaolipwa Mangwasha haukuhudumia familia yake.

iv.Ukosefu wa elimu miongoni mwa vijana. Mangwasha aliwaona vijana wakizurura mtaani.

v.Kutelekeza watoto wa kiume na kuishia kuingilia matumizi ya dawa za kulevya.

vi.Watoto wa kike wanatumiwa katika biashara ya ngono. Sihaba anamiliki danguro anapotumia wasichana wadogo.

vii.Ulanguzi wa mihadarati. Ngoswe anamiliki mtandao wa ulanguzi wa dawa za kulevya.

viii.Matumizi ya pombe haramu. Mrima wanabugia pombe haramu

ix.Ukware. Sagilu anajihusisha kimapenzi na Cheiya ingawa ana mke.

x.Utekaji nyara. Utawala wa Lesulia unamteka nyara Lonare ili asishindane naye katika uchaguzi.

xi.Uharibifu wa mazingira. Viongozi walichimba mchanga na kukata miti bila kujali.

xii.Ufisadi umekithiri katika nchi ya Matuo. Watu wenye ushawishi kama Sagilu hawakulipa kodi na waliagiza hata bidhaa hatari kama maziwa ya watoto yenye sumu.

xiii.Kulikuwa na ukabila. Mangwasha anaeleza jinsi waajiiwa wengi katika ofisi ya chifu walikuwa wa kabila lake mshabaha.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

xiv.Ubaguzi katika ajira. Utawala wa mtemi unawabagua waketwa wakati wa ajira.

xv.Uhaba wa ajira. Vijana wengi waliokuwa wamehafilika kutoka taasisi za elimu walikosa kazi.

xvi.Ukiritimba wa kiuchumi. Sagilu anamiliki nyenzo zote muhimu za kiuchumi

xvii.Unyakuzi wa mali ya umma. Nanzia ananyakua jengo moja refu katikati ya mji.

***zozote kumi (alama 10x1=10)***

c) Majazi

Majazi ni mbinu ya kisanaa ya kuipa sehemu au mhusika katika kazi ya fasihi jina kutokana na sifa, maumbile, tabia au mienendo yake. Baadhi ya wahusika na sehemu mbalimbali zimepewa majina ya kimajazi. Ifuatayo ni mifano ya matumizi ya majazi katika riwaya ya Nguu za Jadi:

i. Matuo: hili ni jina la nchi. Linatokana na kitendo cha kutua, au kutuama, kwa maana ya kutosonga mbele. Nchi hii haisongi mbele kwani inakumbwa na changamoto mbalimbali.
ii. Waketwa: jina hili linatokana na kitenzi 'keta', kumaanisha hali ya kumpiga mtu na kumwangusha. Waketwa ni watu wanaodharauliwa na wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza ingawa tunaambiwa kwamba wana bidii katika masomo na kazi.
iii. Wakule: hawa Wako mbali sana kimaendeleo. Wao wanahodhi nafasi za uongozi nchini Matuo.
iv. Chifu Mshabaha: shabaha ni lengo, kusudi au nia. Huyu chifu ana nia ya kuisambaratisha ndoa ya Mangwasha akishirikiana na Sagilu.
v. Mpenda Bure: huu ni mkahawa unaomilikiwa na Sagilu. Hapa, ndipo wanapokutana Mangwasha na Mrima, ambao wanapendana kwa dhati, japo Mrima ni maskini.
vi. Ponda Mali: hii ni sehemu ambako kunauzwa pombe haramu. Humu ndimo watu kama vile Mrima wanakuja kuharibia pesa zao kwenye vileo hivyo. Wanapondea mali zao humo.
vii. Sihaba: mhusika Sihaba ni mwanamke mwenye mambo si haba (si machache). Yeye ndiye anayetumwa na Sagilu kuja kuvuruga harusi ya Mangwasha na Mrima.
viii. Bwana Mafamba: huyu ni mwanasheria. Maana ya mafamba ni uongo. Mwanasheria huyu ni fisadi na mwongo (uk. 95
ix. Mwamba: huyu ni mwanasheria mahiri sana. Hata Mangwasha anamlinganisha na mlima uliojengwa kwa mwamba. Kutokana na umahiri wake katika sheria, anashinda kesi ya ardhi ya Matango.
x. Majaani: jaa ni mahali panapotupwa takataka. Majaani ni sehemu chafu ambako Mrima anapatikana baada ya kusukumwa kwenye pombe na Sagilu kwa hadaa za pesa.
xi. Mashauri: hili ni jina la kimajazi. Lombo anamwambia Mashauri, "l say, Mashauri. Ninaona leo una mashauri ya kufanya na mzee wako..." (uk. 134).

*za kwanza sita (6x1=6)*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Ushairi**

6.a) Shairi huru/guni (alama 2x1=2)

b) Uchungu – kwa kuwa anakabiliana na mambo mengi yanayomkatisha tama.

Masikitiko (alama 2x1=2)

c) Shairi linazungumzia hali ya kukata tamaa katika maisha.

Anatamani maisha yamwendee vizuri. (alama 2x1=2)

**Zozote mbili kila,hoja alama moja**

d i) Kupanda..kushuka. (Tanakuzi)

ii ) Ghafla nakumbuka ilivyosema ….(Mbinu rejeshi)

iii) Taswira ya mtu aliyechoka. (Taswira) (alama 3 x 1 = 3)

e).Kusisitiza au kutilia mkazo hali aliyoko mshairi.

Kuonyesha utamaushi wa maisha kwa mshairi. (alama 2x1=2)

f).Anaamini kuwa lazima aendelee kujikaza ilikukabiliana na kila hatua mpya ya maisha.

Nijilazimishie na kujiburuta/kujiburarа kuifuata barabara yenye giza na unyevu.

Hata mkishikwa na kujuta kwa mitego hiyo kwa kweli nitafika mwisho wake.

Ikiwa mwisho/hatima yangu haitaufikia kabla/mbele

(alama4 x 1=4)

g).Atoe mifano ya mishata katika shairi.

Mwalimu akadirie mifano ya mishata.

Mf. Ghafla nakumbuka ilivyosema. (alama 2x1=2)

h) Shairi limegawika katika beti.

Halina mpangilio maalum wa vipande.Kipande kimoja tuu.

Kila mshororo una mizani tofauti na mwingine

Halina mpangilio wa vina. (alama 3 x 1 = 3)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

7.a) **Maswala ambayo mwandishi wa shairi hili alidhamiria.**

a i) Maonevu-naeleza anavyoonewa

ii)Vifo-Anaonyesha jinsi wanyonge wanavyokufa

iii)Maangamizi-naonyesha jinsi wanyonge wanaangamizwa.

iv)Tamaa na ubinafsi-naonyesha jinsi matajiri walivyo na tama licha ya kuwa wanazo vya kutosha.

iv) Utabaka (ya kwanza manne alama 4x1=4)

b) Eleza kwa kutoa sababu bahari ya shairi hili ukuzingatia vina,kibwagizo ,idadi ya vipande na mishororo

Msuko - lenye kibwagizo fupi:naandika!

Ukawafi – lina vipande vitatu, ukwapi, utao, mwandamizi

Tarbia – lina mishororo mine katika kila ubeti

Ukara –vina vya nje vinafanana *(zozote nne)* (alama 4x1=4)

c) Mbinu za kutosheleza mahitaji ya kiarudhi

Inkisari – kwacho badala ya kwa hicho , kwayo badala ya kwa hayo

Tabdila – vumiliyo badala ya vumilio

Mazida *(zozote mbili).* (alama 2x1=2)

d) Eleza mbinu za kimtindo alizotumia mshairi

Kinaya-hawa huwapa unene watukufu wenye nayo

Swali balagha- …..kwa hayo unayo? (za kwanza mbili) (alama 2x2=4)

e) Lugha nathari

Wao na si wengine, wanazidi kuangamia huku wakiwapa wakwasi utajiri Zaidi, wangali kwenye dhiki wajitafutiayo. Naandika! *(alama 4x1=4)*

f) Toni katika shairi

Ushauri

masikitiko *(alama 2x1=2)*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**Hadithi Fupi:Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingineo.**

**8. Fadhila za Punda**

a) Maneno ya mwandishi.

Anayerejelewa ni Lilia

Mahali ni nyumbani kwa Luka/Lilia.

Ni baada ya kupigwa na mumewe kwa kumripoti katika kituo cha polisi.

*(alama 4x1=4)*

b) i) Uhuishi/tashihisi-maumivu yakamvamia.

ii) Urudiaji/takriri-fahamu. *(alama 2x2=4)*

**c) Mbinu za kutambua sifa za mhusika.**

i) Ayasemayo mhusika

ii) Matendo ya Mhusika

iii) Wasemayo wahusika wengine

iv) Maelezo ya mwandishi au msimulizi *za kwanza nne (alama 4x1=4)*

a) Kwa kurejelea hadithi “Fadhila za punda” onyesha ufaafu wa mdokezo wa methali ufuatao: ***maskini akipata makalio hulia bwata*** kwa kutolea mifano mwafaka hadithini.

i) Kirukanjia anamsaliti Luka kwa kukosa kumtembelea hospitalini baada ya kujulishwa na daktari huenda asiweze kutembea tena licha ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi naye.

ii) Luka anaachiwa kanisa na pastor Lee Imani baadaye anauza kanisa ili awanie ugavana.

iii) Lilia anampenda Luka na anamshawishi babake akubali kuwabariki lakini Luka anamsaliti Lilia anapokuwa gavana kwa kumpiga makofi na teke la tumbo.

iv) Luka anamsaliti pastor Lee baada ya kumkubali na kufadhili elimu, baadaye anakuwa na uhusiano na mtoto wake anayemtesa baadaye.

v) Luka anawasaliti waumini kwa kuuza kanisa na kuingia siasani.

vi) Luka anamtendea uovu mkewe anapokosa kuandamana naye kwenye kampeni na kumtusi kuwa amenona kama nguruwe na kwamba wanawake ni wengi.

vii) Luka anawasaliti wananchi waliomchagua kwa kutotimiza ahadi alizowatolea wakati wa kampeni.

viii)Luka anamsaliti mkewe kwa kuwa na uhusiano ka kiruka njia. *(alama 8x1=8)*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes